The United Republic of Tanzania
Prime Minister's Office
National Economic Empowerment Council

12 Kivukoni Front
P.O. Box. 1734 Dar-Es-Salaam
Tel: +255 22 2137362
Tel /fax : +255 22 2125596
Email : neec@uwezeshaji.go.tz
Website: www.uwezeshaji.go.tz

12 Barabara ya Kivukoni
S.L.P. 1734 Dar-Es-Salaam
Simu: +255 22 2137362
Simu/Nukushi: +255 22 2125596
Barua Pepe : neec@uwezeshaji.go.tz
Tovuti : www.uwezeshaji.go.tz

**TAARIFA KWA UMMA**

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) linapenda kuchukua fursa hii kuwatangazia wadau wote wa uwezeshaji kutoka kwenye Wizara, Idara, Taassi za Umma na Sekta binafsi kuhusu Kongamano la nne la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambalo litafanyika tarehe 15 juni 2019 katika ukumbi wa Hazina Mjini Dodoma.

Mgeni rasmi wa Kongamano hili anatarajiwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Kassim Majaliwa (MB) ambaye atazindua ripoti ya mwaka ya uwezeshaji wananchi kiuchumi na kutambua wadau wa uwezeshaji waliofanya vizuri kutoka kwenye Wizara na Taasisi za Umma,Mikoa na sekta binafsi kwa kuwapa tuzo za vikombe na vyeti.

Kongamano la mwaka huu linabeba ujumbwe wa 'Wezesha Watanzania Kujenga Viwanda'.

Wakati wa Kongamano kutakuwa na mada mbalimbali ambazo zitaibuliwa na waendesha mijadala ili kushirikishana uzoefu katika masuala ya uwezeshaji wananchi na hasa katika eneo la viwanda.

Baraza linawakaribisha wadau wote wa uwezeshaji kuhudhuria kongamano hili lenye shabaha ya kuhamasisha ushiriki wa wananchi, sekta za umma na binafasi katika kukuza uchumi wa nchi kupitia viwanda.

Imetolewa na;

**Bi. Beng'i Issa**

**Katibu Mtendaji,**

**10 Juni, 2019**